


Agizo la Kaunti ya King ya kuvalia Maski/Barakoa ndani ya majengo itakamilika tarehe 11 Machi, 2022.



Hiyo ina maana gani kuanzia tarehe 12 Machi?

Maski/Barakoa hazitahitajika tena katika maeneo mengi ya ndani ya majengo ya umma:


- Shule, vituo vya kuwatunza watoto na maktaba
- Mikahawa na Baa
- Nyumba za ibada/kuabudu
- Maeneo ya kufanyia mazoezi, vituo vya burudani na maeneo ya ndani ya kushiriki riadha
- Maduka ya kuuzia vyakula, Biashara na maduka ya rejareja






Maski/Barakoa bado zinahitajika:

- Katika maeneo ya kutoa huduma za afya na matibabu, ikijumuisha hospitali, vituo vya kuwatibu watu wasiolazwa, vituo vya kutibu meno na maduka ya dawa
- Maeneo ya utunzaji wa muda mrefu
- Usafiri wa umma, tekisi, huduma za gari zinazoagizwa kwa kutumia simu (mahitaji ya serikali)
- Vituo vya kurekebisha tabia



Biashara za kibinafsi, mashirika, shule na maeneo ya kuwatunza watoto bado yanaweza chagua kutekeleza mahitaji yao kuhusu Maski/Barakoa.

Tafadhali heshimu maamuzi ya watu ya kuendelea kuvaa maski/barakoa.





Kwa nini sasa?

Kaunti ya King inatamatisha agizo lake la kuvalia maski/barakoa ndani ya majengo kwa msingi wa kuendelea kupungua kwa idadi ya watu wanaolazwa hospitalini na idadi ya kesi za ugonjwa kupungua, kulingana na vipimo na mwongozo wa hivi majuzi wa CDC, na viwango vya juu vya watu kupata chanjo



Public Health
Seattle & King County





Nini kinafuata?

Mabadiliko haya ya sera hayamaanishi kuwa ugonjwa wa COVID-19 umekwisha.

Asante kwa kuendelea kuzuia maenezi ya COVID-19 kwa:

- Kupata chanjo na kupata chanjo ya nyongeza ikiwa unastahiki
- Kuboresha uingizaji wa hewa ndani ya majen go
- Kupima na kukaa nyumbani wakati unahisi kuwa mgonjwa
- Kuvalia maski/barakoa ikiwa uko katika hatari ya kuambukizwa COVID-19, ukiwa karibu na watu ambao wamo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi, au katika mazingira yenye watu wengi ambapo inaeleweka

